Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

ISSN: 2663-9289

Volume: 02 Issue: 01 | Dec-2020|
Received: 01.12.2020; Accepted 02.12.2020; Published on 15.12.2020 at www.editoncpublishing.org
Wekesa, W. M., et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, *Double –Blind Peer Reviewed Journal*

# Nafasi Ya Fasihi Simulizi Katika Kuwasilisha Ujumbe Kisheria: Mfano wa Uendeshaji Kesi Za Kitamaduni Miongoni Mwa Babukusu

**Winnie Musailo Wekesa[1]; Dkt Fred Wanjala Simiyu[2]; Dkt. Opande Nilson Isaac[3]**

**[1.] Idara ya Lugha na Elimu ya Fasihi, Chuo Kikuu cha Masinde Muliro, Kenya.**

**[2]Idara ya Kiswahili na Lugha zingine za Kiafrika, Chuo Kikuu cha Kibabii, Kenya**

**[3]Idara ya Lugha, Isimu na Fasihi, Chuo Kikuu cha Kisii, Kenya**

**Main author email: wwekesa2@gmail.com**

## IKISIRI

Utafiti uliazimia kubainisha nafasi ya Fasihi Simulizi katika kuwasilisha ujumbe kisheria. Ulionyesha namna vipengele bainifu vya Fasihi Simulizi vinaweza kutumika kuwasilisha ujumbe kisheria. Ulifanya hivyo kwa kuegemea uendeshaji wa kesi kitamaduni miongoni mwa jamii ya Babukusu. Ili kuafikia lengo hili utafiti ulitumia mbinu ya kithamano. Idadi lengwa ya utafiti ilikuwa jumla ya kesi za kitamaduni tulizohudhuria na kuzirekodi. Utafiti ulijumuisha mbinu ya uteuzi wa sampuli kimaksudi. Uteuzi wa sampuli kimaksudi ulitumiwa kuchagua Chifu, naibu wa Chifu, mwenyekiti wa baraza la wazee na makala maalum yaliyoandikwa kuhusu Fasihi Simulizi na Sheria. Nao uteuzi wa sampuli kinasibu ulitumiwa kuteua mabaraza ya wazee na ya Chifu tuliohudhuria. Waaidha, uchunguzi ulihusisha mbinu za uchambuzi wa yaliyomo, usaili na uchunzaji-shiriki. Njia hizi zilitumika kukusanya data nyanjani na maktabani. Matokeo ya utafiti yalichanganuliwa kithamano. Hii ni mbinu ya kuchanganua data ambayo mtafiti anaeleza na kufafanua matokeo ya utafiti wake kimaelezo. Uchunguzi huu vilevile uliongozwa na nadharia ya Mwingilianomatini. Kwa mujibu wa kesi tulizohudhuria, utafiti ulibaini kuwa kuna vipengele vya Fasihi Simulizi ambavyo vinaoana na hali ilivyo katika taaluma ya Sheria wakati wa uendeshaj kesi kitamaduni miongoni mwa jamii ya Babukusu. Kwa hivyo ni muhali kusema kuwa matini za Kifasihi Simulizi huwa zinachota, kunukuu, kugeuza, kuiga kwa namna ya kufumba, kubeza au kurejelea kwa njia moja ama nyingine matini za Kisheria. Hali kadhalika tanzu zenyewe za Fasihi Simulizi zinaingiliana na kuchangiana katika kutimiza mahitaji ya jamii kupitia shughuli mbalimbali.

**Maneno muhimu:** Nafasi, fasihi simulizi, kisheria na ujumbe.

-----------------------------------------------------------------***-----------------------------------------------------------------

**How to cite this article in APA (6th Edition)**

Wekesa, W. M., Simiyu, F. W. & Opande, N. I. (2020). Nafasi Ya Fasihi Simulizi Katika Kuwasilisha Ujumbe Kisheria: Mfano wa Uendeshaji Kesi Za Kitamaduni Miongoni Mwa Babukusu. *Editon Cons. J. Kiswahili,* 2(1), 173-187

-----------------------------------------------------------------***-----------------------------------------------------------------



© 2020, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

ISSN: 2663-9289

Volume: 02 Issue: 01 | Dec-2020|
Received: 01.12.2020; Accepted 02.12.2020; Published on 15.12.2020 at www.editoncpublishing.org
Wekesa, W. M., et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, *Double –Blind Peer Reviewed Journal*

**UTANGULIZI**

Tanzu nyingi za Fasihi Simulizi hufumba maana katika uwasilishwaji wake. Wataalam wengi wa Fasihi Simulizi ya Babukusu wanaelekea kukubaliana kuwa taaluma hii ina vipengele vifuatavyo; *chingano*, *kimienya*, *chisimo*, *kiminayi* na *kimilukha*. Mara kwa mara kesi zinapoendeshwa katika jamii hii matumizi ya vipengele hivi ilikuwa ni kwa makusudi mbalimbali. Mojawapo ya sababu hizi ni kuwa lugha teule na iliyofumbwa inayojitokeza katika vipengele hivi wakati wa kuwasilisha mitazamo ya kijamii. Ufiche huu wa lugha uliwasilishwa kupitia kwa kufumba maana katika tanzu anuwai zinazotumiwa. Hali dhahiri ni kwamba vipengele hivi vilitumiwa kuwasilisha ujumbe wa kisheria kisawasawa. Mtafitiwa mmoja alilinganisha ufumbaji wa maana katika muktadha wa kitamaduni na lugha ya Sheria inayotumika kortini na wanasheria. Hivi ni kwamba lugha hiyo ya sheria kwa mtu wa kawaida huwa si rahisi kuielewa bila ufafanuzi wa kina. Upambanuzi huu wa kina ulisaidia kufahamu kikamilifu kinachozungumziwa ili kuepuka utata wowote ambao unaweza kuibuka. Hata hivyo tofauti ni kwamba katika lugha teule ya Babukusu, ufumbaji wa maana si kwa ajili ya kumtatanisha mhusika katika kesi bali lengo kuu huwa ni kupunguza makali ya maneno ikilinganishwa na namna ambavyo yangetumika katika lugha ya kawaida. Kwa kufanya hivyo maadili yalidumishwa kwa sababu maneno ya kawaida yanaweza kutoa ujumbe kwa uzito usioweza kustahimilika. Hali hii ni tofauti na lugha ya Sheria ambapo mawakili hutumia lugha hiyo kuwakanganya wahusika katika kesi na nia ya kushinda kesi kila mmoja akivutia upande wake. Wanafanya hivyo kwa sababu umaarufu wao unatokana na idadi ya kesi walizosimamia na zikafaulu hivyo kuwapa wateja katika kazi yao. Kadri wanavyowakanganya watu zaidi ndivyo umaarufu wake unavyozidi hivyo inakuwa muhali kwao kutumia lugha kwa manufaa hayo. Ndiyo sababu mawazo ya Scott (1976) yalikuwa muhimu, anaposema kuwa matumizi ya semantiki katika kazi na uhakiki wa fasihi yanaonyesha majukumu ya lugha katika fasihi. Jukumu mojawapo la lugha ni kutumia jazanda. Uwasilishaji wa dhana kutumia lugha kijazanda ni kutumia lugha kimafumbo ili kuwasilisha ujumbe. Kazi za fasihi zina zaidi ya maana moja katika uhuisano wa kimwimo na hata kimlalo. Tofauti za kimlalo zinaweza kuhusishwa na tofauti zinazojitokeza miongoni mwa hadhira ya kazi ya fasihi. Ilihali tofauti za kimaana kimwimo ni zile maana mbalimbali amabzo anazipata msomaji mmoja anapolinganisha viwango na aina za maana kuhusu suala hilo moja.

**MAPITIO YA Maandishi**

**Nadharia ya utafiti**

Utafiti huu ulielekezwa na Nadharia ya Mwingilianomatini iliyoasisiwa na Julia Kristeva (1966). Mwingilianomatini ni moja ya nadharia za fasihi ambayo hutumika katika kuchunguza na kuchambua data za utafiti linganishi wa kazi za fasihi na nyinginezo. Kristeva (1980), Wamitila (2002), Njogu na Wafula (2007) na Ndumbaro (2013), wameelezea zaidi kuhusu nadharia hii iliyoasisiwa na Mwanasemiotiki wa Kifaransa, Julia Kristeva (1966). Kwa hivyo nadharia hii ilitumiwa ili kupenyeza maana iliyofichika katika tanzu za Fasihi Simulizi kwa kuonyesha muktadha maalum ambamo kipengele mahususi kimetumika na namna kinavyoibua maana iliyokusudiwa. Dhana ya mwingilianomatini ni ya jadi, tangu mwanzo wakati historia ya binadamu na diskosi zinazohusu matini zilipoanza kuwepo. Mara nyingi imefafanuliwa kama seti ya kihusiano iliyopo katika matini inayohusiana na matini au diskosi ya taaluma nyingine katika mawanda ya kitamaduni. Mwananadharia Kristeva anaamini kuwa, mwingilianomatini ni uzalishaji wa maana ndani ya matini na wala sio ndani ya mahusiano kati ya matini mbalimbali. Matini huzaliwa kutokana na unukuzi unaotokana na



© 2020, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

ISSN: 2663-9289

Volume: 02 Issue: 01 | Dec-2020|
Received: 01.12.2020; Accepted 02.12.2020; Published on 15.12.2020 at www.editoncpublishing.org
Wekesa, W. M., et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, *Double –Blind Peer Reviewed Journal*

matini tangulizi, mahusiano ndani ya matini husika na matini nyingine. Kila matini au usemi hudokeza mahusiano ya matini tangulizi kupitia kwa unukuzi wa matini iliyopitwa na wakati. Kwa hivyo, taaluma zinaingiliana kimatini katika kukamilishana na ni vigumu kuziwekea mipaka bayana katika uamilifu wake. Maoni haya yanaungwa na Finnegan (1992) ambaye anasema kuwa maana katika matini inayomilikiwa na umma na kutolewa kwa masimulizi hupatikana ndani ya msururu wa sauti na maneno kando na sauti ya mnenaji.

Asili ya mwingilianomatini kama nadharia hakikifu na mwelekeo wa kuchanganua matini ulitokana na wananadharia watajika kama vile Mikhail Bakhtin na Roland Barthe. Kristeva aliizua nadharia hii ya Mwingilianomatini kutokana na mawazo yaliyoibuliwa na nadharia ya Usemezano ya Mwananadharia Mrusi Mikhail Bakhtin (1895 – 1975). Bakhtin katika nadharia hiyo ya Usemezano, anaamini kuwa kazi ya fasihi ina sauti mbalimbali zinazoingiliana na kupiga mwangwi katika kazi nyingine zilizotangulia, zilizopo au zitakazokuja baadaye. Hii ina maana kuwa, athari ya kazi moja huweza kuonekana katika kazi nyingine zilizotangulia, zilizopo na hata zijazo. Nadharia hii iliibuka baada ya umuundo, ubadili na ile ya usasa na kubadilisha dhana ya matini.

Mwananadharia mwingine maarufu ambaye pia ametoa mchango kuhusu dhana ya mwingilianomatini ni Roland Barthes (1981). Huyu ni msomi maarufu wa Kifaransa katika masuala ya uhakiki wa fasihi na usemi. Maandishi yake yamejitokeza kama changamoto kwa uhakiki wa fasihi. Anazungumzia mwingilianomatini kwa kulenga uasili, maana na suala la ukweli kuhusiana na matini. Kwake matini ni rasilimali za kiuandishi katika kazi fulani. Matini ni kitendo cha kuandika. Analinganisha matini na kazi kisha kusema kuwa 'kazi' ni kwa mikono ilihali 'matini' ni kwa lugha. Barthes ameibua maoni kuwa matini sio chombo kilichojitenga au kilicho na maana moja, bali ni dhana iliyo wazi kwa tafsiri mbalimbali. Kimsingi kiungo muhimu katika mchango wake kuhusu mwingilianomatini ni namna anavyoeleza asili ya matini. Ameipambanua kama dhana inayoweza kuchanganuliwa kwa kuhusisha nadharia za kiisimu na zile za uchunguzi wa kisaikolojia huku zikihusishwa na athari zake kwa matini husika. Anakubaliana na Kristeva kuwa maandishi yaliyoandikwa sasa na ya baada ya usasa yanaweza kuitwa matini kwa sababu yamewekwa wazi ili kufanyiwa tafsiri na fasiri mbali mbali.

Nao Plotell na Charney (1978) wanasema kuwa dhana ya mwingilianomatini husisitiza kwamba matini zote za kisanaa zinaweza kuchukuliwa kama matini moja kuu ambazo huwa zinajibizana, kila moja ikisemezana na nyingine kwenye usemezano uliotanuliwa. Aidha, matini zote huhusiana kwa njia moja au nyingine, na vilevile matini zenyewe hutegemeana ili kuzalisha maana. Maoni haya yanatupa taswira kuhusu nadharia hii kama anavyotuelekeza Kristeva kuwa mwingilianomatini ni kama jumla ya maarifa na mbinu zinazoifanya matini fulani kuwa na maana, ambapo maana ya matini huangaliwa kama inayoitegemea maana inayotokana na matini nyingine katika kile kinachoitwa "mwanda wa ki – mwingilianomatini". Hivyo basi, kwa mujibu wake, matini yoyote ile huchota au kufaidi kutokana na matini nyingine pamoja na kuziumbua zile matini nyingine katika uwanda huo wa kimwingilianomatini.

Mhimili wa nadharia hii ulioongoza utafiti huu unadai kuwa, matini zinaingiliana na kuchangiana, kwa hivyo kuamini kuwa matini moja inajitegemea ni kupotoka. Pamoja na hayo mwingilianomatini huhusisha pia mitindo fulani ya kiusemi na misimbo ambayo imesaidia katika uashiriaji wa kazi za baadaye. Hivyo basi mwingilianomatini sio urejeleaji wa kazi fulani katika kazi nyingine tu, bali pia ni ule mwingiliano wa mitindo ya kiuashiriaji. Kazi kwa mujibu wa wananadharia hii



© 2020, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

ISSN: 2663-9289

Volume: 02 Issue: 01 | Dec-2020|
Received: 01.12.2020; Accepted 02.12.2020; Published on 15.12.2020 at www.editoncpublishing.org
Wekesa, W. M., et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, *Double –Blind Peer Reviewed Journal*

mwingilianomatini ni matokeo ambayo hutumika na kwa upande mwingine matini ni mchakato unaoibuliwa kutokana na kazi. Jambo la pili kuhusiana na mhimili huu ni kwamba nadharia hii inampa msomaji njia anuwai za kupambanua matini pamoja na kazi za fasihi. Hii ni kwa sababu inaangalia kazi za fasihi sawa na matini, kwamba ni tokeo la wazi lililo na uhusiano wa matini nyingine. Lugha ya fasihi kwa kiasi kikubwa huwa ni ya kiishara kwani maana huwa imefumbwa katika semi zinazotumiwa, sawa na lugha ya kisheria. Matini za kifasihi simulizi huwa zinachota, kunukuu, kugeuza, kuiga kwa namna ya kufumba, kubeza au kurejelea kwa njia moja au nyingine matini za kisheria.

**Uhakiki wa maandishi**

Kwa mujibu wa *Oxford Research Encyclopedias* kuhusu Isimu ni kwamba uchunguzi kiisimu wa fasihi simulizi hurejelea namna ambavyo lugha imepangiliwa na kutumika katika sanaa iliyo zungumzi. Hii ina maana kwamba kuna muundo ambao huongezwa kwenye lugha, kubadilishwa na kuwekwa katika makundi tofauti tofauti ili kuleta maana iliyokusudiwa. Mipangilio hii huwa na kiasi fulani, baadhi yake huibuliwa kijumla au kutoka kwa muundo maalum wa kiisimu katika lugha. Hata hivyo miundo ya kiisimu inaweza kukarabatiwa ili kuzua lugha ya fasihi. Miundo hiyo inayoongezwa, ile iliyofanyiwa uchunguzi sana ni ile inayohitaji maneno ya matini kupangwa katika msitari. Muundo huu huhusisha hesabu ya mambo yasiyo ya kiisimu na mdundo wa kimfumo, ambao huchukua mifumo ya kawaida ya fonolojia.

Doke (1948) amezungumzia fasihi na maandishi katika lugha za Kibantu. Anasema lugha ina malighafi yake katika Fasihi Simulizi ya jamii ambayo huathiri matumizi yake. Hivi kwamba ubora wa lugha hizi za Kibantu unatokana na wingi wa msamiati wake. Idadi kubwa ya msamiati huu hutumika katika shughuli za kawaida za wanajamii. Licha ya kuwa msamiati huu hauhusishi mambo na mawazo ya kitamaduni, lugha za Kibantu zimedhihirisha kuwa zinaweza kukopa na kukubali maneno ya kigeni. Hali ambayo inapelekea lugha hizi kuwa na msamiati mwingi. Lugha na jamii ni mambo mawili ambayo hayawezi kutenganishwa, kwani lugha ndiyo hufafanua jamii. Kwa hivyo utafiti huu utabaini matumizi teule ya msamaiti wa Fasihi Simulizi ya Babukusu ikizingatiwa kuwa hii ni mojawapo ya lahaja za lugha za Kibantu. Msamiati huu ndio unaounda vipengele anuwai vya Fasihi Simulizi ikiwa ndio utamaduni wao.

Fortune (1962) anasema kuwa kando na muundo wa lugha kimsamiati na kimofolojia, kuna vipengele vingine zaidi vinavyowasilisha ujumbe. Aidha maudhui yanaweza kuwasilishwa kupitia ishara ambazo hugusa hisia za watu. Mfumo huu hutumika na wasemaji wazuri ambao pamoja na ufundi wa lugha, wao huhusisha ishara na uteuzi mwafaka wa maneno ili kuafikia lengo lao. Miondoko hii huenda sawa na hisia za msemaji. Mtaalam huyu amengazia lugha teule ya wanenaji jambo ambalo linaendana na utafiti huu. Usemaji bora ni kipawa ambacho kinahusu ulumbi kikiwa kipera cha Fasihi Simulizi kinachohusu umahiri katika unenaji. Ulumbi kwa mujibu wa utafiti huu unaweza kuzua utata wakati kesi zinapoendeshwa hivyo kuhitaji ufafanuzi. Ndio sababu utafiti huu utatalii kipengele cha ulumbi kwa juhudi za kuonyesha ni jinsi gani kinavyoweza kutumika kama njia ya kuzua utata wakati kesi zianapoendeshwa kitamaduni miongoni mwa Babukusu.

Fish (1990) akirejelea Sheria na Fasihi Simulizi ya Wagiriki anasema taswira tunayopata kutokana na utamaduni wa jamii hii inahusu mikutano ya hadhara, maamuzi ya kesi, malipo mbalimbali na utatuzi wa migogoro. Katika kauli hii tunaona mwingiliano wa utamaduni na Sheria miongoni mwa Wagiriki. Hali kadhalika amezungumzia mandhari na matukio ya vipengele alivyotaja, ambapo anasema utukiaji wake huwa kinyume na matarajio hasa



© 2020, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

ISSN: 2663-9289

Volume: 02 Issue: 01 | Dec-2020|
Received: 01.12.2020; Accepted 02.12.2020; Published on 15.12.2020 at www.editoncpublishing.org
Wekesa, W. M., et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, *Double –Blind Peer Reviewed Journal*

kuhusiana na namna shughuli za sheria, mahakama, majaji na haki zinavyotekelezwa. Aidha amerejelea matini ya *Homeric* ambayo katika jamii ya Wagiriki yanaonyesha jinsi korti za kitamaduni zilivyochangia kuleta amani, utulivu na kusawazisha mambo kwa wanajamii wote. Mwelekeo ulichukuliwa ulihusisha ukaguzi wa ana kwa ana. Katika kipindi hicho wengi wa watu hawakujua kusoma na kuandika lakini wanajamii waliishi na kuingiliana vyema na wale waliojua kusoma hata kuandika. Vilevile katika miaka ya mwanzo mwanzo mwa kipindi cha kizazi cha kati, stakabadhi zilizoandikwa ziliweza kuwasilishwa kortini zikiandamana na ushahidi ulionenwa na kurekodiwa moja kwa moja. Usawa baina ya utafiti huu na wetu ni kuwa kuna dhana ya kuonyesha mwingiliano wa kitaaluma wa Fasihi Simulizi na Sheria. Hata hivyo kuna tofauti kutokana na jamii zinazohusika kwa Fish (k.h.j.) ameangazia Wagiriki lakini sisi tutarejelea jamii ya Babukusu na hilo tu bali pia katika kuonyesha namna kesi zinavyoendeshwa tutadhihirisha jinsi zinavyoweza kutatuliwa na kupata muafaka bila kufikishwa kortini.

**MATOKEO YA UTAFITI**

Fasihi Simulizi ni taaluma ambayo ina uhusiano wa karibu na utamaduni wa jamii yoyote ile. Utamaduni wa jamii ndiyo hutoa taratibu zinazoendesha shughuli za kila siku na mahusiano ya watu katika jamii husika. Lugha ikiwa ni sehemu ya utamaduni huo. Msokile (1992), anasema Fasihi Simulizi ni kazi ya sanaa inayotumia lugha. Kazi hii ya sanaa huhifadhiwa katika ubongo na kusambazwa kwa njia ya masimulizi ya mdomo. Kwamba Fasihi Simulizi ndiyo aina ya pekee ya sanaa inayotumia lugha kujitambulisha au kujitofautisha na aina nyigine za sanaa. Fasihi Simulizi ni mfumo unaoweza kuainishwa na kuchanganuliwa katika tanzu zinazojitegemea na kujikamilisha kiutendakazi kwa kuingiliana na taaluma nyinginezo. Fasihi Simulizi ya jamii ya Babukusu ambayo ndicho kigezo kilichorejelewa katika utafiti huu imeshughulikiwa na wataalamu mbalimbali kwa njia tofauti tofauti. Mwingilianomatini katika kazi za Fasihi Simulizi na Sheria ni suala ambalo limekuwa likijitokeza sana katika shughuli anuwai za kijamii. Utafiti ulibaini kuwa uhusiano uliopo baina ya taaluma ya Fasihi Simulizi na Sheria, ndio ulipelekea ofisi ya Chifu kufanya kazi karibu sana na korti/mahakama. Ni kutokana na hali hii ndiyo sababu utapata kwamba kesi zilizunguka baina ya korti; afisi ya chifu na baraza la wazee. Hii inaoana na mawazo ya Posner (1998) ambaye amejadili kuhusu usomaji wa sheria katika vyuo vikuu hivi sasa na anasema unafuata mkondo wa kimwingiliano; ambapo sheria si sehemu ya taaluma ya falsafa bali ni sayansi ya kijamii. Vilevile kutokana na mtazamo wa kitamaduni uliongia katika kipindi cha baada ya usasa, nadharia za kisiasa na kiuchumi zikawa zimeingizwa katika uhalisia mpya wa kisheria. Mtaalam huyu anazidi kusema kuwa wasomi wa kisasa wanataka kuunganisha usomaji wa taaluma ya Sheria na masomo ya sanaa kisha kutambua majukumu ya lugha na Fasihi katika kuunda maadili ya jamii.

Kuambatana na matokeo ya utafiti huu Chifu alitoa mfano mwafaka kuhusu kesi ya deni. Kwamba aina hii ya kesi wakati mwingine ilitatiza na ikawa watu wanazungukia kitu kimoja kidogo hivyo kupoteza muda wa korti. Hizi ni miongoni mwa kesi ndogondogo ambazo mahakama inapendekeza kuwa zitatuliwe kule mashinani na ukoo. Kuna wadeni ambao walisumbua katika kulipa. Kesi aina hii zilishughulikiwa katika kiwango cha afisi ya Chifu, kwenye mabaraza ya wazee na katika mivigha kama vile *lufu*. Maelezo hayo yalithibitishwa zaidi kutokana na kesi kuhusu deni tuliohudhuria kama watafiti**.** Wakati mwingine huwa ni kwamba kesi ilisikizwa na makubaliano yakawepo ya jinsi ya kulipia deni hilo lakini anayedaiwa akakosa kutimiza. Inapofikia kiwango hicho basi wahusika waliekezwa kortini ili kuruhusu sheria ichukue mkondo wake. Fish (1990) akirejelea Sheria na Fasihi Simulizi ya Wagiriki anasema taswira tunayopata



© 2020, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

ISSN: 2663-9289

Volume: 02 Issue: 01 | Dec-2020|
Received: 01.12.2020; Accepted 02.12.2020; Published on 15.12.2020 at www.editoncpublishing.org
Wekesa, W. M., et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, Double –Blind Peer Reviewed Journal

kutokana na utamaduni wa jamii hii inahusu mikutano ya hadhara, maamuzi ya kesi, malipo mbalimbali na utatuzi wa migogoro. Katika kauli hii tunaona mwingiliano wa utamaduni na Sheria miongoni mwa Wagiriki.

Hali kadhalika Fish (k.h.j.) huyu amezungumzia mandhari na matukio ya vipengele alivyotaja, ambapo anasema utukiaji wake huwa kinyume na matarajio hasa kuhusiana na namna shughuli za sheria, mahakama, majaji na haki zinavyotekelezwa. Amerejelea matini ya *Homeric* ambayo katika jamii ya Wagiriki yanaonyesha jinsi korti za kitamaduni zilivyochangia kuleta amani, utulivu na kusawazisha mambo kwa wanajamii wote bila upande wowote kutoka pale na hisia za kuonewa. Hii ndio sababu afisi ya chifu ililazimika kutumia ujanja kumusukuma anayedaiwa kulipa deni hilo. Chifu na baraza lake waliweza kufanya hivyo kwa kuongeza faida kwa kila mwezi kwenye deni hilo ili kumsukuma anayedaiwa kulipa haraka. Ikiwa anayedaiwa aliendelea kusumbua, anayedai alishauriwa kutafuta msaada wa wakili. Anamwendea wakili kutumia stakabadhi za maelewano kutoka kwa chifu.

Nia ya kuu ya kumhusisha wakili katika kudai deni huwa ni kwa sababu yeye ataweka mtaji wake na hii ina maana kiasi cha deni kitaongezeka. Hizi zote zikiwa ni juhudi za kuhakikisha kuwa deni linalipwa. Hivyo anayedaiwa alipokea barua kutoka kwa wakili ambapo alijiwasilisha kwa wakili ili aweze kujieleza. Katika kujieleza anapaswa kusema ni kwa namna gani ataweza kulipa deni hilo. Hivyo wakili humpa muda kulingana na makubaliano. Iwapo mdaiwa hatatimiza aliyoyasema basi wakili alilazimika kuwasilisha kesi hiyo kortini ikiwa kama kesi ya jinai. Kesi nyingi zilishughulikiwa na afisi hii ya chifu na wenyeviti wa koo na wazee. Katika kuendesha kesi hizi lugha teule ilitumika. Kwa kutumia lugha hii teule maana ya mambo na hali huwa haijitokezi waziwazi bali ilifumbwa katika vipengele kama vile methali, misemo, vitendawili, ngano, mashairi na nyimbo.

**Methali**

Kesi tulizohudhuria zilionekana kutumia kipengele hiki zaidi kuliko vile vingine. Methali zilitumika kutekeleza majukumu mbalimbali kama kutahadharisha, kuonya, kutia moyo, kuhamasisha, kikashifu, kuadilisha na kukuza uhusiano mwema katika jamii.

Hivyo basi baadhi ya methali ambazo zilitumika katika uendeshaji kesi kutokana na matokeo ya utafiti zilidhamiria kutahadharisha kwa mfano;

> *Nandakambilwa kakona khumwanda kwa enjoli.*

Maelezo ya maana na matumizi ya methali hii ni kuwa, *nandakambilwa* ni mtu ambaye haambiliki wala hasemezeki. Mtu ambaye hazingatii mawaidha au ushauri, daima anatenda mambo visivyo na akishauriwa habadiliki. *Kakona* ina maana kulala kwa, *khumwanda* ni barabara kubwa na pana, *kwa* ni kwenye nayo *enjoli* ni fisi. Ni methali ambayo maana yake ya juu ni mtu ambaye hatilii maanani mashauri anayopewa hujipata kalala kwenye barabara wanayopitia fisi. Maana ya ndani ni kuwa mtu asiyesikia mawaidha mara nyingi hujipata ameingia kwenye shida kubwa zaidi. Hivyo ilikuwa inawahimiza wahusika katika kesi hiyo kusuluhishia mambo yao hapo ili kuepuka gharama na uhasama unaoweza kutokea kufuatana na maamuzi ya korti. Methali hii ilikuwa na maana inayoshabihiana na methali ya Kiswahili inayosema kuwa *asiyesikia la mkuu huvunjika guu*. Mtu ambaye haambiliki au hasemeki aliishia kujipata pabaya. Kukosa kuzingatia mawaidha na ushauri kutoka kwa watu wengine hasa waliokuzidi kwa umri kunaweza kumtia mtu matatani. Methali hii ilitokea katika kesi iliyohusu deni. Lugha iliyotumika katika methali hii ni ya



© 2020, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

ISSN: 2663-9289

Volume: 02 Issue: 01 | Dec-2020|
Received: 01.12.2020; Accepted 02.12.2020; Published on 15.12.2020 at www.editoncpublishing.org
Wekesa, W. M., et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, *Double –Blind Peer Reviewed Journal*

kimafumbo na ilihitaji kupambanuliwa. Tulipomuuliza Chifu iwapo wahusika wote katika kesi walielewa maana ya methali hiyo. Alijibu kuwa wakati mwingine wahusika walikosa kuelewa maana hivyo kulikuwa na miktadha ambayo ufafanuzi ulitolewa ili wanaohusika wapate maana kamili. Hii ilikuwa ni kwa ajili ya kuhakikisha kuwa kila mhusika anashiriki bila kuhisi kwamba amebaguliwa.

Hali kadhalika katika kesi za kutoa tahadhari kulitokea matumizi ya methali;

> *Engila sebolela okenda ta* (barabara haisemi na anayetembea)

Maneno yaliyojenga methali hii yana tafsiri ifuatayo; *engila* ni barabara, *sebolela* ni haimwambii ilhali *okenda* anayetembea na *ta* hapana. Maana yake ni kwamba mtu anapokuwa anatembea barabara haimuambii anakoenda wala kilicho kule mbele anakoelekea. Ni methali ambayo ilitokea katika kwenye hadithi ya wasichana walioenda katika shamba la jitu na kuchuna mboga zake. Hadithi hii ilitokea katika utendaji wa *lufu.* Ilionekana kwamba wale wasichana walikuwa na mazoea ya kuenda katika shamba la jitu na kuchuna mboga zake lakini siku hii hawakujua yaliyokuwa yanawasubiri huko. Njia waliokuwa wakiitumia kila mara ingewaambia yaliyokuwa mbele yao bila shaka siku hiyo hawangeenda huko. Kurejelea muktadha wa maisha ina maana kuwa hatuwezi kuyatambua maisha na hali zetu za baadaye kwa sasa. Ingekuwa hivyo watu wangetahadhari na kujiepusha na shida. Kwa hivyo hali tunazokumbana nazo baadaye ni majaliwa ya Mwenyezi Mungu. Unapotembea barabarani mbele unakoenda hukujui wala kufahamu ni yapi yanayokusubiri lakini nyuma unakotoka unajua yale uliyoyaona. Kwa hivyo jamii ya marehemu waliambiwa methali kutokana na hoja kuwa baba mzazi alikuwa ametembea nao safari ya maisha kufikia pale. Sehemu ya maisha yao iliyosalia wangetembea bila yeye hivyo ilihitaji tahadhari kwa sababu hakuna aliyejua ya mbeleni. Methali nyingine iliyotumika kutahadharisha ni ile inayosema kuwa;

> *Omwana nakhetuyile saria khukenda ta* (Mtoto asipojikwaa hataogopa kutembea)

Mara nyingi watu wanapenda kujifunza kutokana na hali zinazoathiri maisha yao moja kwa moja. Methali hii ilitumiwa kuwatahadharisha vijana na watoto. Kwamba wanapokanywa kuhusu jambo fulani hawasikii mpaka pale wanapopatwa na janga ndipo waamini. Msamiati unaounda methali yenyewe una tafsiri ifuatayo; *omwana* ni mtoto, *nakhetuyile* ni asipojikwaa, *saria* ni hataogopa *khukenda* ni kutembea kisha *ta* ni kikanushi. Ni methali ambayo ilitumiwa katika kesi zilizohusu upataji wa uja uzito nje ya ndoa hasa kwa vijana. Vijana wa jinsia zote waliohusika katika kesi aina hii walikosolewa na kukaripiwa kwa kutumia methali hii. Mwenyekiti wa kikao kimoja cha kesi ya aina hii alitumia methali hii kurejelea Nakhumicha msichana ambaye alikuwa amepachikwa mimba na Situma. Anamwambia sasa baada ya kujikwaa mvulana amemkana na hiyo inakuwa kama tahadhari kwake na wasichana wengine.

Vilevile katika uendeshaji kesi kulidhihirika matumizi ya methali zilizotia moyo. Methali hizi zilihimiza watu kutokata tamaa katika juhudi zao za maisha kama vile;

> *Lisae liambusia namwikhalwa* (uzao ulimvukisha mtu kwa jina Namwikhalwa)

Tafsiri ya maneno katika methali hii ni kama ifuatavyo; *lisae* ni uzao au uwezo wa kuzaa, *liambusia* ni kuvukisha nalo *namwikhalwa* ni jina la mtu ambaye kwa kukosa uzao alichekelewa na kudharauliwa. Maana ya methali hii ni kwamba mtu ambaye alikosa watoto alidharauliwa na wanajamii wengine. Baada ya kupata watoto unakuwa na usemi na kutengewa nafasi muhimu katika jamii. Mtendaji wa mivigha ya lufu katika kesi moja tuliohudhuria



© 2020, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

ISSN: 2663-9289

Volume: 02 Issue: 01 | Dec-2020|
Received: 01.12.2020; Accepted 02.12.2020; Published on 15.12.2020 at www.editoncpublishing.org
Wekesa, W. M., et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, *Double –Blind Peer Reviewed Journal*

alihusisha methali hii katika mazungumzo yake. Methali ilitumika kushauri watoto wa marehemu kuendeleza sera zake. Hatua ambayo yeye hakuifikia wao waifikie miradi ambayo aliacha waimilizishe na mengine. Methali na misemo ni vipengele ambavyo vilimpa mtendaji lugha safi ya kutumia kadamnasi ya watu. Ni lugha ya mnato na kutoa ujumbe kwa namna ya kuvutia. Mchakato huu unaoana na Lloyd (1964) ambaye anaeleza kuwa kuna mtazamo unaodai kuwa Sheria ya awali ya miaka kabla ya kuzaliwa kwa Kristo, kama vile Sheria kumi za Musa (Torah) zilidhihirisha vipengele vya kitamaduni vya Wayahudi na hii ilizifanya kuwa karibu sana na Fasihi Simulizi kuliko Sheria. Hata hivyo Sheria hizi za Musa hazikuwa za kutumika katika mazingira ya kortini bali ziliendesha shughuli za maisha ya Wayahudi sawa na taratibu za kiserikali. Hivyo anasema utamaduni wa jamii usichukuliwe kuwa ni mazoea tu bali ni taratibu zilizokubaliwa ili kuongoza shughuli na mahusiano ya jamii husika. Jamii fulani huenda ikakosa kuwa na serikali inayoongozwa na Sheria maalum, bali ikawa kinachoendesha na kuratibu mambo na shughuli zake ni mila na desturi za jamii hiyo. Hii ilichangia kukubali kuwa utamaduni wa Babukusu ndio uliendesha shughuli za maisha yao kabla na baada ya kuingia kwa taratibu za kiserikali.

> *Lituli lifumilanga eunwa elimo* (zizi la ng'ombe hupata sifa kutokana na fahali aliye mle ndani)

Tafsiri ya maneno ya methali hii ni kama ifuatavyo; *Lituli* ni zizi la ng'ombe, *lifumilanga* linapata sifa kwa sababu ya, *eunwa* ni fahali na *elimo* aliye katika zizi hilo. Ni methali ya kibukusu iliyotumiwa mhusika wa kiume katika kesi kwa kumhimiza achukue nafasi yake katika boma. Kwamba atapata sifa kutokana na ubora wa boma lake. Vilevile boma litapata sifa njema kwa ajili ya mume mwenye boma hilo. Methali hii ilitumiwa na mama mmoja katika kesi baina ya Kizito na mkewe Nekesa. Kesi hii ilihusu mgogoro wa ndoa baina ya wawili hawa. Mume alihimizwa kuwa yeye ndiye wa kutoa mwelekeo katika boma lake, kwa mkewe na watoto. Mwelekeo ambao utaiwezesha jamii yake kusimama na kuwa bora. Ilitumika wakati ambapo kuna lawama kuhusu utepetevu wa mwanamume, amekosa kuwajibika kwa hali na mali katika familia.

Hali kadhalika matumizi ya methali yalikusudia kukuza maadili mema katika jamii. Hivyo basi methali ifuatayo ilitumika kutimiza wajibu huo;

> *Lirima lira ne selisuta ta* (hasira inaua lakini haibebi)

Tunaweza kulinganisha methali hii na ile ya Kiswahili inayosema *hasira hasara*. Tafsiri ya maneno katika methali hiyo ni kama ifuatavyo; *Lirima* ni hasira, *lira* ni inaweza kuua, *ne* ni lakini, *selisuta* ni haibebi ilhali *ta* ni kikanushi. Ina maana kwamba hasira ni mbaya na inaweza kuua lakini haibebi. Hii ilikusudia kuhimiza wanaozozana kupunguza hasira katika tofauti zao. Hasira inaweza kumsukuma mtu kutenda jambo baya ambalo laweza kuleta madhara makubwa hata kifo. Methali hii ilitumiwa katika mazishi ya mama alieuawa na mumewe kutokana na ugomvi wa kinyumbani. Katika maziko ya mama huyo aidha, kulikuwa na istilahi zingine nyingi za Fasihi Simulizi ya Babukusu zilizotumika. Kwa hivyo ushauri ulikuwa kwamba kunapotokea hali ya kuvutana ni muhimu kuweza kudhibiti hasira. Isiwe kwamba ndiyo inayokuongoza kwa sababu mtu akiwa na hasira hawezi kufanya maamuzi mazuri. Kuna wakati ambapo watu waliopigana na kuumizana kutokana na kutoelewana kuhusu jambo fulani, utapata kuwa wanashinda wakitishiana maisha na wanapokutana lazima wakwaruzane. Mzozo na kisasi ni mambo yaliyotokana na hasira ambayo badala ya kuleta utangamano ilifanya watu kutengana hata zaidi. Kuna watu ambao hasira zao



© 2020, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing
Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)
ISSN: 2663-9289
Volume: 02 Issue: 01 | Dec-2020|
Received: 01.12.2020; Accepted 02.12.2020; Published on 15.12.2020 at www.editoncpublishing.org
Wekesa, W. M., et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, *Double –Blind Peer Reviewed Journal*

hazirudi chini. Hawa wanaweza kusababisha madhara ambayo yangeepukika kwa kupunguza hasira.

Vilevile kuna hii methali inayosema kuwa *Khuayaya khwakila namususuni walea kumunwa.* Nayo pia ilikusudia kukuza maadili mema. Ni istilahi iliyojitokeza hapa na pale katika uendeshaji wa kesi kitamaduni. Kwa mfano ilitokea katika mojawapo ya kesi ya kutowajbiika kwa mume katika ndoa yake. Maneno yanayounda methali hii yana maana zifuatazo; *Khuayaya* ni kuhangaika huku na kule, *khwakila* ni kulimfanya, namususuni ni jina la aina ya ndege mwenye mdomo mrefu, *walea* nalo ni kurefuka na *kumunwa* ni mdomo. Kwa hivyo maana ya methali hii ni kwamba kutotulia kulimfanya ndege anayeitwa *namususuni* kurefuka mdomo. Kwa hivyo iwapo Kizito hatatulia na kuhakikisha anaishughulikia familia yake angekuja kujipata taabani. Tabia hii inaweza kumtia mashakani labda angeiharibu familia, kusambaratisha ndoa yake, kumdhuru mkewe au hata kugonganisha watu. Kwa hivyo ni vyema kuwa na utulivu katika maisha ili mtu asije akajipata taabani.

Methali nyingine iliyojitokeza katika shughuli za uendeshaji kesi ilikuwa; *Buike bwakila ekhafu yeyakalila kumunwa.* Hii nayo ilitumika kwa ajili ya kuonya dhidi ya tamaa. Hapa ni kwamba lazima ilimfanya ng'ombe akajikuna kutumia mdomo wake. Kuna hali ambazo zinaweza kukulazimu kufanya jambo la ajabu na kushangaza lisilowezekana katika hali ya kawaida. Ng'ombe kujikuna kutumia mdomo si jambo rahisi lakini ni lazima maana ndiyo njia ya pekee kwa ng'ombe huyo kuweza kufanya kitendo hicho. Vilevile mtu anaweza kukumbwa na hali ngumu ambayo itamsukuma kufanya jambo lisilo la kawaida. Kitambo watu walihifadhi mazao kama vile mahindi, mtama, wimbi ghalani. Mtu kutokana na njaa akaamua kwenda kuchota chakula kutoka ghala la mwenzake bila idhini yake kisha akakamatwa. Alijitetea kutumia methali hii kuonyesha amekubali makosa yake lakini haikuwa kupenda kwake ila ni hali ambayo haingeweza kuepukika. Kuwa hali ngumu ya mikeketo ya njaa ndiyo iliyompelekea kufanya kitendo hicho. Kwa hivyo yule mshitaki atashawishiwa kumsamehe kutokana na sababu kwamba aliyechukua nafaka yake kutoka ghalani, alilasimishwa na hali ambayo hangeweza kuiepuka. Kwamba isingekuwa njaa iliyokuwa imembana, basi asingechukua nafaka ile. Kama ilivyojadiliwa awali ni kuwa katika hali zote za jamii hii, utatuzi wa kesi ya namna hii au yoyote ile ilikuwa ni kwa ajili ya kuleta mapatano. Kwa hivyo mshtakiwa anaweza kuchukuliwa hatua kama vile kwenda kufanya kazi katika shamba la mshtaki bila malipo lakini baada ya kazi labda apewe tu kitu cha kula tu sio kubeba.

Methali nyingine iliyonuia kuonya ilikiwa ni, *rebanga Kitimule wanyowa ebuyumbu*, ina maana kuwa ni vyema kuuliza waliokutangulia katika kufanya jambo lolote. Huenda ikawa ni katika ndoa, shughuli za kikazi na nyinginezo. Waliotangulia wana tajriba ya maisha na hivyo wanaweza kukuelekeza. Maana ya maneno katika methali hii ni *rebanga* ni zoea kuuliza, nalo *Kitimule* ni jina la mtu, *wanyowa* ni aliyetangulia kufika na *ebuyumbu* jina la moja wapo ya ukoo miongoni mwa jamii ya Babukusu. Ilitumiwa kwa mtu ambaye alijiona kuwa anajua sana kuwapita wenzake hata walio na umri mkubwa ama waliomtangulia katika kufanya jambo fulani. Anaweza kudhani kuwa amefika kumbe ndio safari inaanza. Methali hii inaweza kulinganishwa na msemo wa Kiswahili unaosema *mwanzo ndio mkoko unaalika maua.* Ilimhitaji mtu kuchukua muda wa kulifikiria na kulielewa jambo kabla ya kulikimbilia. Hii ilitumika katika kesi anuai mfano inajoitokeza katika kesi ya uja uzito wa Nakhumicha kwa kumtahadharisha Situma. Waliowahi kushuhudia hali kama hiyo na wakaona matokeo yake humuambia methali hii. Ama kuonya mtu anayeingia katika ndoa kwenye familia iliyo na maadili mabaya k.v wauaji, wachawi, wenye chuki na wezi.



© 2020, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

ISSN: 2663-9289

Volume: 02 Issue: 01 | Dec-2020|
Received: 01.12.2020; Accepted 02.12.2020; Published on 15.12.2020 at www.editoncpublishing.org
Wekesa, W. M., et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, *Double –Blind Peer Reviewed Journal*

**Tashbihi**

Kando na methali matumizi ya lugha teule ya Kibukusu pia yalisheheni tashbihi ambazo ziliafiki masuala anuwai ya kijamii ikiwemo utatuzi wa kesi. Tashbihi zilitumiwa kutolea picha fulani kwa njia ya ulinganishaji. Zilijumuisha utumiaji wa viungo fulani ili kuzua mwelekeo maalum wa kimaana, badala ya kutumia vielezi au vivumishi tu. Maana za tashbihi zilizotumka zilihitaji kufasiliwa ili zieleweke ipasavyo kwa wahusika wote katika kesi. Pamoja na hayo ziliibua hisia nzito zaidi. Kwa misingi hiyo zifuatazo ni miongoni mwa tashbihi ambazo zilitumika wakati wa uendeshaji kesi kitamaduni. Tashbihi nazo sawa na methali zilitekeleza karibu majukumu sawa. Kwa mfano kwa ajili ya kukuza maadili mema tashbihi ifuatayo ilitumika ;

> *Khukwalala khu mukhasi woo namwe khu musecha woo nga eng'ilisi* (kutulia kwa mkeo ama mumeo sawa na vazi linalokaa mwilini vizuri)

Tafsiri ya maneno yaliyotumika kuunda tashbihi hii ni kama ifuatavyo *khukwalala* ni kunyooka, *khu* ni kwa, nalo *omukhasi* lilimaanisha mke, kisha *woo* ni wako, *namwe* ina maana ya ama, *omusecha* ni mume, *nga* ni kama ilhali *eng'ilisi* ni aina ya nguo ambayo ikivaliwa inakaa mwilini. Tashbihi hii ilitumika kwa kusudi la kuwashauri watoto wa marehemu katika utendaji wa *lufu* kudumisha umoja katika nyumba zao kwa kuwa waaminifu. Istilahi hii ilinuia kumhimiza mtu awe mke au mume kuwa mwaminifu katika ndoa yake. Watu wawe wutulivu katika ndoa zao licha ya changamoto wanazopitia. Uaminifu katika ndoa ni jambo muhimu na hivyo jamii ina jukumu la kuhakikisha kuwa hili linadumishwa.

Aidha, tashbihi zilikuwa na wajibu wa kukuza uvumilivu miongoni mwa wanajamii. Hivyo kulitumika mfano ufuatao wa tashbihi;

> *Khwikhalilikha oli okhama linani* (kuvumilia mithili ya mtu anayekamua jitu)

Hii ni tashbihi nyigine iliyotumika katika kesi baina ya Metrine na Elijah ambayo ilihusu *makanyako*. Makanyako ni hali ambapo mtu anaingia katika shamba la mwingine bila idhini ya mwenye shamba. Maneno katika tashbihi hii yanaweza kutafsiriwa ifuatavyo katika Kiswahili; *Khwikhalilikha* ni kuvumilia, kisha *oli* ni mithili ya, nalo *okhama* ni anayekamua na *linani* ni jitu. Maana ya kipengele hiki ni kuvumilia sawa na yule anayekamua jitu. Kukamua jitu si jambo rahisi wala haliwezekani katika hali ya kawaida ya maisha. Iwapo litatokea basi lilihitaji uvumilivu na ukakamavu mkubwa kabisa. Ni tashbihi iliyotumiwa kumsihi Elijah kutoa msamaha kwa Metrine shemeji yake. Licha ya kuwa alikuwa ameharibu mimea yake na kumsababishia hasara aliombwa amsamehe. Elijah aliona ugumu wa kusamehe bila ya kurejeshewa malipo ya gharama ya fedha alizokuwa ametumia kama alivyoeleza. Kwa hivyo mzee wa kijiji Memba akawa anamsihi kuwa si jambo rahisi lakini ilimbidi kwa sababu shemeji yake hangeweza kupata pesa alizokuwa akidai. Hatimaye Elijah alimsamehe shemeji yake hata hivyo akamtuma awaonye watoto wake na awafunze kuwa na nidhamu.

Matumizi haya ya tashbihi katika utatuzi wa kesi yanaoana na maoni ya mtaalam Scott (1976) ambaye anasema kuwa kila matini ya kifasihi huwa na muundo wake wa diskosi, ambao huhusu kuigawa matini hiyo katika makundi kadha. Fasihi Simulizi ni taaluma ambayo imegawnywa katika tanzu na vipera mbalimbali. Hii inajumuisha kugawa masimulizi katika matukio na



© 2020, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

ISSN: 2663-9289

Volume: 02 Issue: 01 | Dec-2020|
Received: 01.12.2020; Accepted 02.12.2020; Published on 15.12.2020 at www.editoncpublishing.org
Wekesa, W. M., et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, *Double –Blind Peer Reviewed Journal*

kubainisha mipaka ya matukio haya. Matini ya fasihi pia huwa na msamiati teule wa kukopa au wa kubuni maneno na kujihusisha na uchanganyaji fulani wa maneno hayo. Matini hizi pia huwa na ubainifu, yaani namna ambavyo lugha yake inajitofautisha ni wazi. Mitindo hii inaweza kuchukuliwa kuwa ufasiri uliopatikana kutokana na maana zinazochanuzwa na tanzu tofauti tofauti. Hata hivyo kuna mielekeo tofauti ya kimtindo katika Fasihi Simulizi, ambayo huchukulia mitindo hii kwa namna isiyoweza kuathiri maana. Fasihi Simulizi haiwezi kuwa na semantiki au pragmatiki tofauti na ya lugha husika lakini maana yake inaweza tu kuwa ngumu ikilinganishwa na maana ya maneno katika lugha ya kawaida.

**Misemo**

Kama ilivyoelezwa awali *chisimo* miongoni mwa jamii ya Babukusu hujumuisha methali na misemo. Hivyo basi kipengele hiki kwa mujibu wa wasailiwa kiliibua lugha iliyokomaa na yenye tasfida kwa minajili ya kuficha makali ya lugha ya kawaida. Baadhi ya misemo ambayo ilitumiwa katika uendeshaji wa kesi ilikusudia kuadilisha mfano ni; *khukhupa babasio kamasolosi;* maneno katika msemo huu yana maana zifuatazo *khukhupa* ni kupiga, *babasio* ni wenzako na *kamasolosi* ni maneno ya kichinichini. Kwa hivyo katika ujumla wake msemo unamaanisha kuwafitini wenzako mara nyingi kwa wakubwa. Msemo huu ulijitokeza katika mwendelezo wa utendaji katika mivigha ya *lufu* Mtendaji baada ya kutoa hadithi aliutumia ili kuhimiza umoja baina ya watoto wa marehemu. Mfano mwingine katika jamii ni kwamba mtu anaweza kuwa ni kiongozi wa kundi fulani dogo, wakati ambao yuko hapo watu wale wanazungumza naye vizuri na kumpa sifa kemkem. Lakini unapata miongoni mwa watu kuna wanaomsaliti kwa mkubwa. Labda ana kosa fulani badala ya kumwambia wanaitumia kama sababu ya kumfitini. Kwa hivyo msemo huu unawalenga watu ambao wana mazoea ya kupeleka fitina juu wengine bila sababu maalum na wakati mwingine tabia hii ikawaletea balaa.

Vilevile kulikuwa na matumizi ya msemo kwa nia ya kuonya dhidi ya kuwa na haraka. Kwamba haraka inaweza kumkosesha mtu mambo mazuri. Msemo unaosema *mbakala kalia bibisi* ulitumika kuonyesha atahri ya haraka katika maisha. Maneno katika msemo huu yana maana zifuatazo; *mbakala* ni mtu ambaye hana utulivu yuko huku na kule, *kalia* ni alikula ilhali *bibisi* ni vibichi. Msemo huu ulikuwa na maana kwamba mtu ambaye ana haraka sana katika maisha yake hula chakula kibichi. Hana muda wa kusubiri vyakula viive hata kama vinapikwa na havijaiva kwa sababu ya haraka yake atapakuliwa ale na aende. Msemo huu ilidhihirika katika kesi baina ya Nakhumicha na Situma. Ulihimiza kuwa Situma awe mvumilivu na aende pole katika kufanya mambo sio kuamkia tu na kufanya maamuzi ya haraka. Ilikuwa muhimu kwake kujipa muda wa kutafakari kabla ya kuchukua hatua. Msemo ulitumika katika kesi hii kuwasaidia wahusika kutulia licha ya yale yaliyokuwa yamewakumba na kuwtia wasiwasi. Matumizi yake aidha yalikuwa yanawakosoa kutokana na haraka yao ya maisha na uchu wa kutaka kushiriki mapenzi kabla ya kuwa tayari kukubali matokeo yake ambao ni uja uzito. Kwa hivyo mambo katika maisha yalihitaji kuwa na subira. Kwa kuwa *subira huvuta heri*.

Hali kadhalika msemo mwingine ambao ulijotokeza katika mojawapo ya kesi ni *khuandalasia mukhumbo.* Msemo huu ulidhamiria kujasirisha hasa watu wa jinzia ya kiume. Tafsiri ya maneno yaliyounda msemo ni kama ifuatavyo *khuandalasia* ni kukaza sana nalo *mukhumbo* ni mkononi. Msemo huu ulitumiwa kuhimiza utiaji bidii na kukazania katika kila jambo unalolitekeleza. Ilimhitaji mtu kuwa na ujasiri, nguvu na bidii katika kutekeleza mambo yake ndiposa aweze kufaulu maishani. Msemo huu ulitokea katika mwendelezo wa *lufu* katika hadithi ya jitu na wasichana. Ulirejelea mvulana aliyekuwa anamtaka msichana aliyekamatwa na mtego uliotegwa na jitu kumshika mtu aliyekuwa akiiba mazao yake. Matumizi



© 2020, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

ISSN: 2663-9289

Volume: 02 Issue: 01 | Dec-2020|
Received: 01.12.2020; Accepted 02.12.2020; Published on 15.12.2020 at www.editoncpublishing.org
Wekesa, W. M., et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, *Double –Blind Peer Reviewed Journal*

yake yalidhihirisha kwamba mvulana yule alifaulu kumpata msichana aliyenaswa kutokana na bidii ailiyokuwa nayo. Aidha alikuwa jasiri, mwerevu na nguvu za kukabiliana na jitu ili kumnusuru msichana aliyempenda. Tabia ya uzembe ilikashifiwa sana katika jamii.

**Hadithi**
Sawa na tanzu nyingine ngano ni sehemu kubwa ya kuwasilisha jumbe kwa njia ya mafumbo katika jamii nyingi barani Afrika na ulimwengu kwa jumla. Utanzu huu ulitekeleza majukumu anuwai katika jamii ya Babukusu. Isitoshe hadithi hujumuisha tanzu zingine kama nyimbo, methali na misemo katika utambaji wake. Mwanataaluma Tracey (1948) anazungumzia kipera cha nyimbo katika Fasihi Simulizi. Anasema kipengele hiki hutumika pamoja na tanzu nyingine kama vile ngano, mivigha na sherehe mbalimbali. Anaendelea kusema kuwa nyimbo hujitokeza katika nathari ikiwa ni kwenye hadithi, masimulizi, vitendawili na methali. Utukiaji wa nyimbo au uimbaji huwa ni kwa njia ya kutofautisha nathari na ushairi. Hadithi ni utanzu unaoweza kujumuisha aina nyingine za vipera katika kuwasilishwa kwake. Mfano ni hadithi hii iliyosemwa na mtendaji wa mivigha ya *lufu* – sherehe ambayo hufanyiwa wanaume miongoni mwa Babukusu.

Katika utendaji wa mivigha hii ambayo huja siku tatu baada ya kuzikwa marehemu kuna nafasi ya kuangazia masuala yanayohusu deni, ugawaji wa mali ya marehemu, mpaka wa shamba na mengineyo. Shughuli hii iliendehswa sawa na shughuli za kesi kwa sababu kuna wakati kulitokea mvutano baina ya familia na wanajamii wengine. Hadithi iliyotolewa iliangazia tofauti hizo na kutoa tahadhari kwa wahusika wote. Katika kutamba hadithi palitokea pia matumizi ya wimbo hali ambayo ilionyesha mwingiliano wa matini za kifasihi simulizi. Mwendelezo huu unakubaliana na mchango wa mwananadharia Kristeva (1966) ambao unaeleza kuwa mwingilanomatini mara nyingi umefafanuliwa kama seti ya kihusiano iliyopo katika matini inayohusiana na matini au diskosi ya taaluma nyingine katika mawanda ya kitamaduni. Kristeva (k.h.j) anaamini kuwa, mwingilianomatini ni uzalishaji wa maana ndani ya matini na wala sio ndani ya mahusiano kati ya matini mbalimbali. Matini huzaliwa kutokana na unukuzi unaotokana na matini tangulizi, mahusiano ndani ya matini husika na matini nyingine.

**Wimbo**
Nyimbo ni aina ya sanaa katika Fasihi Simulizi ambayo hutumia lugha teule, sauti na kiimbo maalum chenye kuleta mahadhi ya kuvutia wasilikizaji. Nyimbo nyingi huwasilisha ujumbe kwa njia ya mkato na fiche. Uwasilishaji wa Fasihi Simulizi huandamana na matumizi ya ishara na nyimbo miongoni mwa miondoko mingine inayoambatana na utendaji katika Fasihi Simulizi. Kipengele hiki cha wimbo kilidhihirika katika baadhi ya kesi zilizohudhuriwa na watafiti. Wimbo ulitumiwa katika kuwasilisha kilio, kuomba msaada na kukashifu tabia hasi katika jamii. Kwa mfano wimbo ulioimbwa na msichana baada ya kukwama kwenye mtego wa jitu na kumnasa. Wimbo huo ulijitokeza katika hadithi iliyotambwa na kahini katika utendaji wa *lufu*. Katika majibizano hayo jitu liliitika kwa wimbo huo huo baada ya kutambua kuwa mmoja wa wasichana waliokuwa wakija katika shamba lake kuchuna mboga na matunda amekwama kwenye kiti. Sehemu ya wimbo huo inasema hivi;

Msichana: *Khatebee nikho khatebe –*
*mbaambile nolile*
*Eeh mundalo ya wenani –*
*mbaambile nolile*
*Eeh mundalo ya wenani –*
*Khaungu mako*
*Mundalo ya Welikhe –*
*Khaungu mako*



© 2020, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

ISSN: 2663-9289

Volume: 02 Issue: 01 | Dec-2020|
Received: 01.12.2020; Accepted 02.12.2020; Published on 15.12.2020 at www.editoncpublishing.org
Wekesa, W. M., et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, *Double –Blind Peer Reviewed Journal*

*Khatebe khandobora – Khaungu mako*
*Yaba nacha chikhu – Khaungu mako*

Msichana aliyenaswa aliimba wimbo huu ili kuomba msaada anasuliwe kutoka mtego huo. Anasikitika kwamba mtego ulimchagua yeye na kumnasa licha ya kila mmoja wao kukikalia mara kadha. Anadai kuwa yeye alikuwa ameenda kutafuta kuni. Anaimba bila kujua kuwa anajishtaki kwa jitu lenye shamba ambalo baada ya kumsikia akiimba lilianza kuitika likielekea nyumbani ili limpate. Kwa bahati nzuri mvulana aliyekuwa akimtaka msichana huyo naye pia alimsikia akiimba. Mvulana huyu alijaribu kumfikia kabla ya lile jitu. Hata hivyo ilimbidi kukabiliana na jitu lile kwa ujanja kwa sababu tayari lilikuwa linakaribia kufika. Katika makabiliano hayo mvulana huyo aliliua jitu na hivyo kumkomboa msichana na hatari iliyokuwa inamchungulia. Hali hii inakubaliana na maoni ya Wanjala (2015) ambaye katika kazi yake ameangazia mwingilianotanzu unaojitokeza wakati wa utendaji wa mivigha ya *embalu* na *mwaka kogwa.* Akiongozwa na nadharia ya Ujumi wa Kinudhuma na nadharia ya Muono-Ndani ameonyesha namna mwingilianotanzu hujengwa katika mivigha hii kwa kuelekezwa na fanani, hadhira, muktadha na vivigha maalum. Aidha, ilikuwa muhimu kubainisha namna mwingilianotanzu huo huisaidia mivigha ya *embalu* na *mwaka kogwa* kutekeleza wajibu wake. Mwingiliano huu wa vipengele vya Fasihi Simulizi ndio ulioshuhudiwa katika uendeshaji wa kesi miongoni mwa Babukusu kitamaduni.

## Hitimisho

Kwa mujibu wa matokeo ya utafiti imeonekana kwamba mwingiliano taaluma unaodhihirika kati ya Fasihi Simulizi na Sheria unaiwezesha jamii ya Babukusu kukabiliana na hali zinazoikumba. Ni wazi kuwa wakati wa uendeshaji kesi za kitamaduni vipera vya fasihi simulizi ya Babukusu kama vile jazanda, methali, misemo, tashbihi, maghani, mivigha, nyimbo na ngano zilitumika ili kukuza uhusiano bora na maelewano miongoni mwa wanajamii. Katika kutekeleza wajibu huu maana ya vipera hivi huwa imefumbwa kwa lengo la kupunguza makali.

## Mapendekezo

Utafiti huu ulilenga kuchunguza udhihirikaji wa vipengele vya Fasihi Simulizi katika taaluma ya Sheria kwa ujumla. Aidha ulionyesha namna vipengele hivyo bainifu vya Fasihi Simulizi viliwasilisha ujumbe wa kisheria katika kuendesha kesi kitamaduni miongoni mwa Babukusu. Hatukutathmini kwa kina kila kimoja cha vipengele hivyo katika upekee wake. Tafiti za baadaye zinaweza kufanywa ili kushughulikia kina na kiwango cha kila utanzu mahususi katika uendeshaji wa kesi kitamaduni kwa kurejelea jamii yoyote ya Kiafrika. Tanzu za Fasihi Simulizi licha ya kuingiliana kila moja inaweza kujisimamia na kujikamilisha katika upekee wake.

## MAREJELEO

Bakhtin, M. M. (1984). *Problems of Dostoevsky's Poetics.* Minneapolis: University of Minnesota Press.

Bakhtin, M. M. (1986). *Speech Genres and Other Late Essays*. Austin & London: University of Texas Press.

Barthes, R. (1981). From Work to Text. *Textual Strategies: Perspectives in Poststructuralism Criticism*, ed. by Josue Harari V. Ithaca, NY: Cornell University Press.



© 2020, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

ISSN: 2663-9289

Volume: 02 Issue: 01 | Dec-2020|
Received: 01.12.2020; Accepted 02.12.2020; Published on 15.12.2020 at www.editoncpublishing.org
Wekesa, W. M., et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, *Double –Blind Peer Reviewed Journal*

Bassey, M. (1999). Case Study Research in Educational Settings. Nottingham: McGraw-Hill Education (UK).
Cohen, L. na Manion, L. & Keith, M. (1994). *Research Methods in Education.* (6th ed.). London: Routledge.
Creswell, J. W. & Clark, V. L. P. (2007). *Designing and conducting mixed methods research.* Thousand Oaks, CA: Sage Publications.
Doke, J. (1948). *The Basis of Bantu Literature*. Vol. 18, Issue 4. DOI: https//doi.org/10,2307/ published by Cambridge University Press.
Enon, J. C. (1998). *Education Research, Statistics and Measurements*. Kampala: Makerere University
Finnegan, R. (1992). *Oral Literature in Africa.* Nairobi: Oxford University Press.
Fish, S. (1990). Almost Pragmatism: Richard Posner's Jurisprudence. University of Chicago Law Review, 57.
Fortune, J. (1962). *Melon of Ecstasy*. London: Hutchinson. ISBN 978-1853754708
Gay, R. (2000). *Educational Research Conference for Analysis and Application. (Toleo la 4).* New Jersey.
Jwan, J. & Ong'ondo, C. (2011). *Qualitative Research*: An Introduction to Principles and Techniques. Eldoret: Moi University.
Kombo, D.K & Tromp, D.L. (2006). *Proposal and Thesis Writing: An introduction.* Nairobi : Pauline Publications Africa. Linguistics, 12, 180-95.
Kress, G. (2008). Meaniing and Learning in a world of instability. Studies in Philosophy and Education. 27,253-266
Kristeva, J. (1966). *Desire in Language: A Semiotic approach to Literature and Art*. New York: Columbia University Press.
Kristeva, J. (1980). *Desire in Language: A Semiotic approach to Literature and Art*. New York: Columbia University Press.
Lloyd, D. (1964). *The Idea of the Law*. Baltimore: Penguin.
Njogu, K. na Wafula, R.M (1999). *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
Msokile, M. (1992). *Misingi ya Hadithi Fupi.* Dar es Salaam: Dar es Salaam Printing Press.
Ndumbaro, E. (2013). Taathira katika Fasihi: Msingi wa kuwepomotifu za aina moja katika tanzu anuai za Fasihi za mataifa/makabila tofauti tofauti ulimwenguni. Makala katika chombez.blogspot.de/2013/10/taathira-katika-fasihi.html?m=1
Plotell, P. na Charney, H. (1978). *Intertextual Encoding in the Writing of Women's Literary History.*
Computers and the Humanities, 38 (2). Published by Springer.
Posner, R. (1988). *Law and Literature*, revised ed., Cambridge: Harvard University Press.
Powell, D. W. na Conway, G. C. (2004). *Cluster Analysis of Mass Spectrometry Data Reveals a Novel Component of SAGA*. Mol Cel Biol 24.
Robson, C. (2002). *Real World Research*: A Resource for Social Scientists and Practitioner –Researchers (2nd ed.). Oxford: Blackwell Publishers Ltd.



© 2020, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

ISSN: 2663-9289

Volume: 02 Issue: 01 | Dec-2020|
Received: 01.12.2020; Accepted 02.12.2020; Published on 15.12.2020 at www.editoncpublishing.org
Wekesa, W. M., et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, *Double –Blind Peer Reviewed Journal*

Scott, P. (1976). *A General Semantics Approach to the Reading Literature*. A Review of General Semantics. Institute of General Semantics.

Spata, G. (2003). *The Statesman Yearbook: Politics, Cultures and Economics of the World*. Palgrave: Macmillan Ltd.

Tracey, M. (1948). *The Decline and Fall of Public Service Broadcasting and Production of Political Television*. Colorado: University of Colorado Boulder Press.

Wamitila, K.W. (2002). *Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: Phoenix Publishers Ltd.

Wanjala, S. F. (2015). Mwingilianotamzu katika Fasihi Simulizi ya Kiafrika: Mfano wa Embalu na Mwaka Kogwa. Tasnifu ya Uzamifu, Chuo Kikuu cha Kenyatta.



© 2020, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org